

SHINDANO LA INSHA KUADHIMISHA SIKU YA TAKWIMU AFRIKA MWAKA 2019

1.0 Siku ya Takwimu Afrika

Tarehe 18, Novemba kila mwaka Bara la Afrika huadhimisha siku ya Takwimu Afrika. Maadhimisho ya Siku ya Takwimu Afrika chimbuko lake ni uamuzi uliochukuliwa mwaka 1990 kwa pamoja na Kamisheni ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa Afrika na Mikutano wa pamoja wa watakwimu, wataalamu wa mipango na wanademografia wa nchi za Afrika.

2.0 Lengo la Maadhimisho

Lengo kuu la kuasi maadhimisho haya ni kuuelimisha umma katika bara la Afrika kuhusu umuhimu wa takwimu na kuongeza ufahamu kuhusu nafasi na mchango wa tasnia ya takwimu katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii barani Afrika.

2.3 Maadhimisho ya Siku ya Takwimu nchini Tanzania

Tanzania ikiwa mwanachama wa Umoja wa Afrika kila mwaka huungana na wanachama wengine wa Umoja huo kuadhidhimisha siku hii kwa kufanya shughuli mbalimbali ambazo zinaakisi maudhui ya maadhimisho hayo. Miiongoni mwa matukio yatakayoambatana na maadhimisho haya ni mashindano ya kuandika Isha kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini.

2.4.0 Shindano

Lengo la shindano hili ni kuongeza ufahamu kwa vijana kuhusu masuala ya kitakwimu ikiwemo umuhimu na matumizi ya takwimu katika maendeleo. Aidha, kuwashamasisha vijana kupenda tasnia ya takwimu na kuwa mojawapo ya tasnia ambazo zinaweza kuwawezesha kutimiza ndoto zao za maisha.

2.4.1 Mada ya Insha: UMUHIMU WA TAKWIMU KATIKA KUPANGA NA KUIMARISHA ELIMU YA SEKONDARI NCHINI TANZANIA

2.4.2 Urefu wa Insha: ISIZIDI MANENO MIA TANO (500)

2.4.3 Mwisho wa Kuwasilisha Insha: ALHAMISI YA TAREHE 21 NOVEMBA, 2019 SAA 10: 00 JIONI

2.5.0 Kutangaza Washindi

Washindi watangazwa na kupatiwa zawadi zao siku ya kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Takwimu Afrika yatakayofanyika tarehe 28 Novemba, 2019 katika ukumbi wa mikutano wa Kituo cha Mikutano ya Kimataifa cha Julius Nyerere kilichopo Mtaa wa Shaaban Robert jijini Dar es Salaam.

Wasilisha Insha yako kwa anuani zifuatazo:

Ofisi ya Taifa ya Takwimu,
Barabara ya Jakaya Kikwete,
S.L.P 2683,

DODOMA

AU

Ofisi za Takwimu za Mkoa ulipo

AU

Emails: sg@nbs.go.tz na nakala kwa joel.weja@nbs.go.tz, said.ameir@nbs.go.tz,
mateew@gmail.com